

TANGAZO LA SERIKALI Na. 41 la tarehe 24/1/2025

**SHERIA YA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)**

AMRI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA WA MAGARI 5 YA MRADI WA USAID -
AFYA YANU WA M/S DELOITTE CONSULTING LIMITED.

Jina na kuanza
kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa wa Magari 5 ya Mradi wa USAID - Afya Yangu wa Deloitte Consulting Limited na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika kuanzia tarehe 11 Oktoba 2025.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa magari yaliyoainishwa katika Jedwali yanayoingizwa ndani ya nchi au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha kwa niaba ya au na Deloitte Consulting Limited kwa ajili ya kutumika katika mradi wa USAID - Afya Yangu, unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa magari tajwa yatatumika kwa matumizi mengine au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itakoma kutumika tarehe 9 Aprili, 2025.

*Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa wa Magari 5 ya Mradi wa USAID -
Afya Yangu wa Deloitte Consulting Limited*

—————
JEDWALI
—————

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

Na	Maelezo	Namba ya Chesesi	Namba ya injini
1	TOYOTA LANDCRUISER 76 HARDTOP, 10-SEATER, 5 DOORS	JTEEB71J80F022398	1HZ-1026543
2	TOYOTA LANDCRUISER 76 HARDTOP, 10-SEATER, 5 DOORS	JTEEB71JX0F022404	1HZ-1026562
3	TOYOTA LANDCRUISER 76 HARDTOP, 10-SEATER, 5 DOORS	JTEEB71JX0F022371	1HZ-1026328
4	TOYOTA LANDCRUISER 76 HARDTOP, 10-SEATER, 5 DOORS	JTEEB71J30F022387	1HZ-1026446
5	TOYOTA LANDCRUISER 76 HARDTOP, 10-SEATER, 5 DOORS	JTEEB71J90F022409	1HZ-1026610

Dodoma,
31 Disemba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
Waziri wa Fedha